



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**  
**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**



**TAARIFA KWA UMMA**

**MKURUGENZI MKUU LATRA ATOA POLE KWA MKUU WA MKOA WA MTWARA**

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA CPA Habibu Suluo, ametoa salamu za pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mhe. Brigedia Jenerali Marco Gaguti kufuatia vifo vya watu 12 na majeruhi 17 vilivyotokana na ajali mbaya iliyotokea leo tarehe 26 Julai, 2022 eneo lenye mteremko la Mji Mwema, kata ya Magengeni Manispaa ya Mtwara Mikindani mkoani humo.

Ajali hiyo imetokea kwa basi la shule aina ya Toyota Hiace lenye namba ya usajili T207CTS, lenye leseni namba A1A224802 inayoisha tarehe 31 Januari, 2023 kutumbukia kwenye korongo.

Katika salamu zake, CPA Suluo ametoa pole kwa wafiwa wote, amewapa pole majeruhi na kuwaombea uponaji wa haraka.

Aidha, LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani watafanya uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo cha ajali hii na kuchukua hatua kuzuia ajali za aina hii.

**Imetolewa na:**  
**Kitengo cha Mawasiliano – LATRA**  
**26 Julai, 2022**

